



قبر کی پہلی رات

# Usiku Wa Kwanza Kaburini

(Swahili)



Shaikh-e-Taariqat Ameer-e-AhleSunnat

Mwanzilishi wa Dawat-e-Islami,

Allama Moullana Abu Bilal

**MUHAMMAD ILYAS**  
Attar Qadiri Razavi



Dawat-e-Islami

قبر کی پہلی رات



# Usiku Wa Kwanza Kaburini

Kijitabu hiki kiliandikwa na Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Ahl-e-Sunnat, muanzilishi wa Dawat-e-Islami ‘Allāmaḥ Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دامت برکاتُهُمْ عَلَيْهِمْ katika lugha ya Kiurdu. Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Majlise Tarajim. Endapo utaona makosa yoyote katika tafsiri yake au utungaji wake, tafadhali wajulishe Majlise Tarajim kwa njia ya posta au kwa kipepesi ili upate thawabu.

## Majlise tarajim (dawat-e-islami)

Alami Madani Markaz, Faizan-e-Madina,  
Mahalla Saudagran, Old Sabzi Mandi, Baab-ul-Madina,  
Karachi, Pakistan  
Wasiliana kwa nambari: +92-21-34921389 hadi 91  
[translation@dawateislami.net](mailto:translation@dawateislami.net)

## **MAKTABA-TUL-MADINA**

**UK:** 80-82 Bordesley Green Road, Birmingham, B9 4TA.

Contact: 07989996380 - 07867860092

E-mail: uk@dawateislami.net

**USA:** Faizan-e-Madina, P. O. Box 36216, Houston, Tx 77274.

Contact: +713-459-1581, 832-618-5101

**INDIA:** 19/20 Muhammad Ali Road, opposite Mandvi post office

Mumbai – 400 003.

Contact: +91-022-23454429

**BANGLADESH:** K.M Bhovan, 1<sup>st</sup> Floor, 11, Andar Killa Chittagong.

**HONG KONG:** Faizan-e-Madina, M/F-75, Ho Pui Street, Tsuen Wan N.T.

Contact: +85-98750884 – 31451557

**SOUTH AFRICA:** 61A, Mint Road, Fordsburg, Johannesburg.

Contact: 011-838 9099

**KENYA:** Kanz-ul-Iman, Near Al-Farooq Hospital, Tonoka Area Mvita,

Mombasa.

Contact: +254-721-521916

**TORONTO CANADA:** 1060 Britannia Road Unit 20, 21 Mississauga ONT

Canada.

Contact: +141-664-82261

**MOZAMBIQUE:** Mesquita Faizan-e-Madina Rua Alfredo Lawley, Esturro, Beira.

Contact: 00258-848554888 - 00258-822808580

الْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ النَّبِيِّنَّ  
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيمِ

## Du'a Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo.  
ان شاء الله عز وجل utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللّٰهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَانْشُرْ  
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَالْجَلَلِ وَالْأَكْرَامِ

### Tafsiri

Ee mola عَزَّوَجَلَ ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie Mtakatifu kabisa.

(Al-Mustatraf Juzuu I, uk. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Mswalie Mtume ﷺ mara moja kabla na baada ya dua. (Roohani Hikayyat UK. 68)

# *Chati Ya Unukuu*

ء	A/a	ڇ	ڦ/ڻ	ڙ	L/l
ا	A/a	ڇ	Z/z	ڻ	M/m
ٻ	B/b	ڙ	X/x	ڻ	N/n
ڦ	P/p	ڦ	S/s	،	V/v, W/w
ٿ	T/t	ڦ	Sh/sh		
ڌ	ڌ/t	ڦ	ڦ/ڦ	ڦ/ڦ/ڦ	ڪ/ڪ
ڻ	ڻ/ڻ	ڻ	D/d	ڻ	Y/y
ڢ	J/j	ڢ	T/t	ڢ	Y/y
ڦ	Ch	ڦ	Z/z	-	A/a
ڻ	H/h	ڻ	-	-	U/u
ڦ	Kh/kh	ڦ	Gh/gh	-	I/i
ڏ	D/d	ڏ	F/f	ڏڏ	U/u
ڙ	ڏ/ڏ	ڙ	Q/q	ڙڙ	I/i
ڙ	ڙ/ڙ	ڙ	K/k	ڙڙ	AA/aa
ڻ	R/r	ڻ	G/g		

## *Orodha Ya Yaliyomo*

Du'a Kabla Ya Kusoma Kitabu.....	iii
Chati Ya Unukuu .....	iv

## **USIKU WA KWANZA KABURINI ..... 1**

Ubora wa kumswalia Mtume ﷺ .....	1
Makaburi yote huonekana yamefanana (kwa nje) lakini kwa ndani.....	4
Kila mtu ataoomba mauti siku moja .....	6
Tumekuwa duniani kwa utaratibu maalum lakini... .....	7
Atakuwa hajawahi kushuhudia usiku kama huo .....	7
Wasia wa a'la hadrat.....	8
Wasia wa Amīr-e-Aḥl-e-Sunnat.....	9
Machozi ya kipenzi cha mwenyezi mungu .....	9
Kituo cha kwanza baada ya kufa ni kaburi .....	10
Mazishi ni mlinganizi mnyamavu .....	10
Tunavyoogopa giza.....	10
Kisa chenyé mazingatio kuhusu jumba la kifahari .....	11
Wanaoleweshwa na anasa za kidunia .....	12
Udanganyifu wa ulimwengu.....	13
Ishi kama msafiri katika ulimwengu huu .....	14

Sababu za Mwisho Mbaya

Lengo la maisha ya ulimwenguni hasa ni kujitayarisha kwa maisha ya ahera .....	14
Tangazo la maiti .....	15
Usemi wa maiti.....	15
Wito wa kaburi.....	16
Ima ni bustani ya peponi au shimo la motoni .....	17
Huruma ya kaburi kwa mtiifu .....	17
Mwito kutoka makaburi jirani.....	17
Mazungumzo na maiti .....	18
Ziko wapi nyuso hizo nzuri sasa? .....	19
Fanya maandalizi sasa .....	19
Muimbaji alijiunga vipi na Dawat-e-Islami? .....	21
Niliota kuhusu majina mazuri 99 Ya Allah ﷺ .....	24
Maua 14 ya Madani kuhusu Mavazi .....	25
Pambo la ki Madani.....	28
Dua ya attar .....	29

الْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعَلَمِيْنَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ  
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطَنِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيمِ

## Usiku Wa Kwanza Kaburini

Shetani bila shaka atakuzuia kusoma kitabu hiki kinachoeleza usiku wa kwanza kaburini-tafadhali zishinde hila hizi za shetani.

### Ubora wa kumswalia Mtume ﷺ

Mtume Mtukufu amesema, “Kuniswalia mimi ni mwangaza katika Sirāṭ. Anayeniswalia mimi mara 80 siku ya Ijumaa, atasamehewa madhambi yake ya miaka 80.” (*Al-Jāmi'-uṣ-Saghrīr*, uk.320, *Hadis 191*)

صَلُوْا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّدٍ

Tabi'i maarufu, walii Sayyidunā Ḥasan Basrī عليه رحمه الله القوي wakati mmoja alipokuwa amekaa katika kizingiti cha mlango wake ulipita msafara wa waombolezaji kwenda kuzika. Katika msafara huu kulikuwa na msichana mdogo aliyekuwa akikimbia huku akilia sana na akipiga mayowe, “Ewe babangu mpendwa!

Wakati huu ulionijia leo sijawahi kuukabili awali.” Sayyidunā Ḥasan Basrī ﷺ aliposikia sauti hiyo ya huzuni, akaanza kulia, moyo wake ukawa na wahaka na kwa huruma akauweka mkono wake juu ya kichwa cha msichana yule yatima mwenye huzuni na akasema, “Ewe mwanangu! Hakika ni marehemu babako wala si wewe ndiye ambaye leo anafikiwa na hali ambayo hajaikabili tangu hapo awali.”

Siku iliyofuata alimuona msichana yule yule mdogo akilia huku akielekea maziarani. Sayyidunā Ḥasan Basrī ﷺ naye akamfuata na akajificha nyuma ya kichaka ili kupata mazingatio. Msichana mdogo aliweka mashavu yake mchangani huku akilia na kusema, “Ewe babangu mpenzi! Ilikuaje siku yako ya kwanza kaburini kwenye giza bila ya mwenzio wa kuliwazana katika huzuni.

Ewe babangu mpenzi! Jana usiku nilikuwashia taa, nani atakuwa amekuwashia taa kaburini? Ewe babangu mpenzi! Jana usiku nilikutandikia kitanda nyumbani, nani atakuwa amekutandikia kitanda chako kaburini? Ewe babangu mpenzi! Jana usiku nilikukanda mikono na miguu nyumbani, nani atakuwa amekukanda mikono na miguu kaburini? Ewe babangu mpenzi! Jana usiku uliposikia kiu nilikupa maji ya kunywa, nani atakuwa amekupa maji kaburini? Ewe babangu mpenzi! Jana usiku nilikufunika mwili wako kwa blanketi, nani atakuwa ameufunika mwili wako kaburini? Ewe babangu mpenzi! Jana usiku nilikufuta jasho usoni, nani atakuwa amekufuta jasho kaburini? Ewe babangu mpenzi! Mpaka jana usiku nilikuwa

nikija kila uliponiita, utakuwa umemuita nani kaburini na akaja kukuhudumia? Ewe babangu mpenzi! Jana usiku ulipokuwa na njaa nilikuletea chakula, utakuwa umeletewa na nani kaburini? Ewe babangu mpenzi! Mpaka jana nilikuandalia vyakula mbalimbali, Nani atakuwa amekuandalia kaburini?

Aliposikia maneno hayo ya kuhuzunisha kutoka kwa msichana mwenye huzuni, Sayyidunā Ḥasan Basrī عَلَيْهِ مَحَمَّدًا الْكَوْنِي akaanza kulia na baada ya kumsogelea msichana yule, akasema, “Ewe mwanangu! Usiseme hivyo; sema, “Ewe babangu mpenzi! Wakati ulipozikwa uso wako ulielekezwa kibla. Je, uso wako umeelekea huko huko au umegeuzwa upande mwengine? Ewe babangu mpenzi! Ulipozikwa ulifunikwa kwa sanda safi nyeupe ambayo haikuwa na mchanga. Je, bado ni safi na hijaingia mchanga? Ewe babangu mpenzi! Uliwekwa kaburini mwili wako ukiwa mzima. Je, mwili wako bado ni mzima au wadudu wameshaua? Ewe babangu mpenzi! Wanavyuoni wakiislamu wanasema kuwa katika usiku wa kwanza, maiti huulizwa maswali juu ya imani yake; wengine huweza kujibu ilhali wengine hushindwa.

Je ultoa majibu sahihi au ulishindwa? Ewe babangu mpenzi! Wanavyuoni wanasema kaburi huwa kunjufu kwa baadhi ya watu ilhali kwa wengine huwabana. Je, kaburi lako limekuwa namna gani? Ewe babangu mpenzi! Wanavyuoni wanasema kuwa sanda ya wengine hugeuzwa kwa ya peponi ilhali ya wengine hubadilishwa kwa ya motoni. Je, sanda yako imebadilishwa kwa ya peponi au motoni? Wanavyuoni wanasema kuwa kaburi

Usiku wa Kwanza Kaburini

huwapiga pambaja baadhi ya watu kama vile mama anavyompiga pambaja kwa mapenzi mtoto wake aliyepotea ilhali wengine huwabana kwa nguvu na kuwavunja mbavu mpaka zikapishana. Je, kaburi lilikupiga pambaja kwa mapenzi kama mama au likubana na kukuvunja mbavu? Ewe babangu mpenzi! Wanavyuoni wanasema kuwa maiti akishazikwa, hujutia moja ya mambo mawili. Ikiwa alikuwa mwema, hujuta kwa nini hakuongeza mema yake; Ikiwa alikuwa muovu, hujutia maovu yake. Ewe babangu mpenzi! Je wewe ulijutia kutenda mema kidogo au kutenda dhambi? Ewe babangu! Kufikia jana nilipokuita uliitika. Sina bahati leo ambapo nimesimama mbele ya kaburi lako nakuita lakini siwezi kusikia jibu lako. Ewe babangu mpenzi! Umeniondokea kwa njia ambayo hatuwezi kukutana mpaka siku ya hukumu. Ewe Mola mwenye kurehemu ﴿عَزَّوْجَل﴾! Usininyime nafasi ya kukutana na babangu siku ya hukumu.”

Aliposikia maneno ya Sayyidunā Ḥasan Basrī عليهِ سَلَامٌ وَسَلَوةٌ وَرَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوْيِ, msichana huyu mdogo akasema, “Ewe bwana wangu! Maneno yako ya nasaha yamenizundua. Baada ya hapo aliregea na Sayyidunā Ḥasan Basrī عليهِ سَلَامٌ وَسَلَوةٌ وَرَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوْيِ huku machozi yakimtiririka. (Al-Muā’iz al-‘Asfūriyah, uk. 118)

### **Makaburi yote huonekana yamefanana (kwa nje) lakini kwa ndani...**

Ndugu wapenzi waislamu! Nyote mushawahi kuzuru maziara. Je, mumewahi kufikiria ujumbe wa huzuni unaoita, “Enyi

mulioridhika na starehe za dunia hii! Kila mmoja wenu siku moja atakuja (mahali) hapa pa upweke. Kumbuka makaburi haya yanayoonekana kuwa yamefanana kwa nje, si lazima yawe yamefanana kwa ndani. Ndiyo! Ikiwa aliyoko ndani alikuwa akiswali kwa wakati, akifunga mwezi wa Ramadhan, akifanya Itikaf mwezi mzima wa Ramadhan au angaa siku kumi za mwisho, akitoa zaka iwapo imemlazimu, akitafuta riziki ya halali na akikinai na kile alichoruzukiwa, akisoma Qur'an, akiswali Tahajjud, Ishraq, Dhuha na Awwabin, alikuwa mnyenyeketu na mwenye tabia nzuri, akiweka ndevu kulingana na sheria, akivaa kilemba, alikuwa mfuasi wa sunnah, akiwasheshimu wazazi, akichunga haki za watu, akimpenda Allah ﷺ na Mtume wake kipenzi ﷺ, akiwapenda maswahaba na Ahlul baiti na Auliyyaa basi kwa rehema ya Allah ﷺ kaburi lake ambalo kwa nje ni kifusi cha mchanga, kwa ndani huenda likawa na ukubwa wa upeo wa macho na dirisha la pepo likiwa wazi na ndani yake huenda ikawa ni bustani la peponi.

Kwa upande mwengine ikiwa aliyezikwa ndani ya kifusi hakuwa akiswali, kwa kusudi hakufunga Ramadhani, akiwasumbua waislamu wakati wa Ramadhan katika ibada zao au kuwaharibia usingizi wao (kwa kupiga kelele kwa ajili ya michezo kwa mfano karata, keramu n.k), alikuwa bahili kutoa zaka ingawa ilimlazimu, alitafuta riziki ya haram, alihusika na rushwa na riba, hakulipa madeni yake, alikunywa pombe, alicheza kamari, alifungua biashara ya kamari na pombe, aliwaudhi waislamu, aliwatisha na kuwapokonya waislamu pesa zao, aliwateka nyara waislamu

Usiku wa Kwanza Kaburini

ili alipwe fidia, alikuwa jambazi, alikuwa mfisidi wa mali ya umma, alifisidi ardhi, aliwadhlumu wakulima maskini, aliwagandamiza watu alipokuwa akitafuta uongozi, alinyoa au alipunguza ndevu kinyume na sheria, alitazama filamu na drama, alisikiliza nyimbo, alikuwa na tabia ya kutukana, alidanganya, alisengenya, alitoa siri za watu, alikashifu watu, aliwafikiria watu vibaya, alikuwa hajali watu, hakuwaheshimu wazazi wake; basi yawezekana chini ya kifusi hiki kilichotulia, (aliyoko ndani) yuko katika hali ya mateso, dirisha la motoni likiwa wazi, moto unafuka ndani ya kaburi, mwilini amemgandamwa na nyoka na nge, naye anapiga mayowe na kelele ambazo sisi hatuwezi kuzisikia.”

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

### Kila mtu ataonja mauti siku moja

Enyi wafuasi wa Mtume! Tazameni makaburi yalivyo na upweke na mutafakari je, mmoja wetu, akiwa hai, anaweza kulala usiku mmoja tu makaburini? Pengine hakuna hata mmoja wetu ambaye aweza kujishajiisha kufanya hivyo. Basi ikiwa tunaogopa kukaa usiku mmoja makaburini katika uhai wetu, basi baada ya kufa, wakati rafiki zetu na jamaa zetu watatuacha na tutakuwa na akili timamu, tutaona na kusikia kila kitu, lakini hatutaweza kusogea au kuzungumza; Tutaishi viyi kaburini katika hali kama hiyo ya kuogofya! La hasha! Hali yetu ni kwamba tunakuwa na hofu hata tukifungiwa ndani ya jumba la kifahari lenye viyoyozi!

Ndugu waislamu wapenzi! Niaminini. Waliomakaburini leo wanatushauri na wanatoa wito: “Enyi watu musiojali! Kumbukeni! Jana sisi pia tulikuwa hapo (duniani) mulipo nyinyi leo na nyinyi kesho mutakuwa hapa (kaburini) tulipo sisi leo. Hakika kila aliyezaliwa humu duniani lazima atakufa. Kila aliyechuma maua ya uhai atadungwa na miba ya mauti. Kila aliyefurahia anasa za dunia mwishowe atapata huzuni ya mauti.

### **Tumekuja duniani kwa utaratibu maalum lakini...**

Ndugu waislamu wapenzi! Bila shaka tumekuja duniani kwa utaratibu maalum yaani aliyetangulia ni babu, halafu baba, halafu mtoto, halafu mjukuu; hata hivyo kwa kifo, utaraibu huu si lazima. Babu mzee huenda akawa hai ilhali kijukuu kichanga huenda akawa amekufa. Nyanya mzaa mama huenda akawa hai ilhali mama ameondoka duniani. Baba huenda akawa yu hai ilhali barobaro wake huenda akapata ajali akafa. Kama vile hawa jamaa zetu walivyokufa, sisi nasi itatubidi tuondoke ulimwenguni siku moja.

### **Atakuwa hajawahi kushuhudia usiku kama huo**

Sayyidunā Anas bin Malik رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema, “Niwaelezee ya mchana miwili na usiku miwili? (1) siku moja atakufikia mjambe kutoka kwa Allah عَزَّوَجَلَّ imma na taarifa ya kufurahisha ya kuridhika kwa Mola wako au taarifa ya kutofurahika kwa Allah عَزَّوَجَلَّ (2) siku ya pili ni ile utakayofikishwa katika mahakama ya Allah عَزَّوَجَلَّ kupokea kitabu cha amali yako. Kitabu hiki utapewa

Usiku wa Kwanza Kaburini

aidha kwa mkono wakulia au wa kushoto. Na usiku miwili ni:  
**(1)** Mmoja ni usiku ambao aliyekufa atakuwa kaburini na kabla  
yake atakuwa hajawahi kushuhudia usiku kama huo. **(2)** Usiku  
wa pili ni usiku wa kuamkia asubuhi wa siku ya hukumu na baada  
ya hapo hakuna usiku mwingine utakaokuja tena. (*Shu'ub-ul-Imān*,  
*Juzuu ya 7, uk.388, Hadis 10697*)

### Wasia wa a'la hadrat

Enyi muliohai leo na kesho wafu! Enyi mutakaoangamia! Enyi  
watu dhaifu! Enyi wanyonge! Enyi musio na nguvu! Enyi watoto!  
Enyi vijana! Enyi wazee! Hakika usiku wa kwanza kaburini  
hauna mchezo. Sayyidi Imam wa Ahl-e-Sunnat, Mujjaddid wa  
Ahl-e-Sunnat, mfufuzi wa sunna, mvunjaji wa bid'a, mwanachuoni  
wa elimu ya sheria za Mungu, muongozo wa imani, chemichemi  
ya baraka, 'Allāmāḥ, Maulānā, Al-Ḥāj Al-Ḥāfiẓ, Al-Qārī Ash-  
Shāḥ Imām Aḥmad Razā Khān عَلَيْهِمَا السَّلَامُ ingawa alikuwa walii  
wa Allah عَزَّوَجَلَّ na mpenzi mkubwa wa Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ

“Baada ya kuzikwa na kusomwa Talqin, mswalieni Mtume kwa  
saa moja na nusu mfululizo mbele ya kaburi upande wa uso  
wangu ulipolekezwa kwa sauti kubwa ambayo naweza kusikia.  
Halafu munikabidhi kwa أَرْحَمُ الْجِنِينَ na muondoke. Ikiwa mutaweza  
kujisumbua, jamaa zangu au marafiki wawili wakae kaburini  
kwangu kwa siku tatu mchana na usiku wakisoma Qur'an tukufu  
na kumswalia Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ mfululizo kwa sauti ambayo

naweza kusikia; لَنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ moyo wangu utazoea maskani mapya. (*Hayāt-e-A'lā Ḥadrat, Juzuu ya 3, uk. 291*)

## Wasia wa Amīr-e-Āhl-e-Sunnat

كَوْنِيَّةُ مُحَمَّدٍ الرَّحْمَنِ عَلَيْهِ سَلَامٌ Kwa kukubaliana na Sayyidī ‘Alā Ḥadrat Amīr-e-Āhl-e-Sunnat ameandika wasia kama huo pia. Imeandikwa katika ukurasa wa 394 wa ‘hotuba za ‘Attar’, kitabu hiki cha kurasa 436 kina sura ya ‘Wasia wa Madani’: “Ikiwezekana, wale wanaonipenda wakae kando ya kaburi langu baada ya kunizika kwa siku 12 au angaa masaa 12 na wanifurahishe kwa kusoma Qur'an, qasida, kuleta dhikri na kumswalia Mtume Nitayazoea maskani yangu mapya. Katika wakati huu musiache kuswali kwa jamaa kama ilivyo katika vipindi vingine.”

## Machozi ya kipenzi cha mwenyezi mungu

Hebu tutafakari juu ya ucha Mungu aliokuwa nao kipenzi chetu Mtume, aliyekombolewa na ni mkombozi wetu صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْهُوَ أَكْبَرُ، صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ juu ya kaburi. Sayyidunā Barā'ah bin 'Āzib amesema, “Tulishiriki katika mazishi pamoja na Mtume Mtukufu صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْهُوَ أَكْبَرُ، صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ alikaa ukingoni mwa kaburi na akalia mno mpaka mchanga ukaloa maji. Halafu yeye akasema, “Jitayarisheni kwa haya.” (*Sunan Ibn-e-Mājah, Juzuu ya 4, uk. 466, Hadīš 4195*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

### **Kituo cha kwanza baada ya kufa ni kaburi**

Amīr-ul-Mumīnīn Sayyidunā ‘Ušmān Ghānī رضي الله تعالى عنه kila alipozuru makaburi alilia mpaka ndeu zake zikaloa machozi. Akaulizwa, “Kwa sababu gani wewe hulii wakati pepo na moto unapotajwa lakini walilia mno makaburi?” Akajibu, “Nimesikia kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa صلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ, “Hatua ya kwanza ya maisha ya baadaye (ahera) ni kaburi; ikiwa mtu ataokoka katika hatua hii basi mambo yanayofuatia ni rahisi. Ikiwa hata okoka katika hatua hii basi yanayofuatia yatakuwa mazito zaidi.” (*Sunan Ibn-e-Mājaḥ, Juzuū ya 4, Uk. 500, Hadis 4267*)

### **Mazishi ni mlinganizi mnyamavu**

Ndugu wapenzi waislamu! Munaona namna gani Sayyidunā ‘Ušmān Ibn-e-Affān رضي الله تعالى عنه alivyokuwa akimcha Allah عَزَّوَجَلَ! Ni mionganoni mwa ‘Asharāḥ Mubasharāḥ (عَشْرَةُ مُبَشَّرٍ) yaani maswahaba 10 waliobahatika kubashiriwa pepo na Mtume صلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ. Juu ya hayo alikuwa akishikwa na hofu kuhusu vitisho, upweke na giza la kaburi na kwa upande mwengine ni sisi ambao tumesahau kabisa makaburi yetu. Ingawa tunaona mazishi siku nenda siku rudi, hatufikirii kamwe siku moja itakuwa ni mazishi yetu. Hakika mazishi yanachukua nafasi ya mlinganizi mnyamamavu kwetu sisi.

### **Tunavyoogopa giza**

Enyi wapenzi wa Mtume Majuto yalioje! Tunawaona wengine wakiteremshwa kaburini lakini tunasahau kuwa siku moja sisi

pia tutateremshwa. Ah! Tudhaifu mno hadi umeme ukikatika mioyo yetu huwa na wasiwasi mkubwa kwa uwoga hasa kama tuko peke yetu. Juu ya yote haya, hatuna wasiwasi kamwe wa giza totoro la kaburini. Tunashindwa kusimamisha swala, kufunga mwezi wa Ramadhan, kutoa Zaka na kutimiza haki za wazazi wetu... Ah! Usiku na mchana tunatenda madhambi. Bila shaka siku ya kifo haibadiliki wala haiwezekani kucheleweshwa. Ikiwa tutaendelea kufanya madhambi namna hii na kifo kikaja kwa ghafla na kikatupeleka kaburini, tutaumaliza vipi usiku wa kwanza kaburini?

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

### Kisa chenye mazingatio kuhusu jumba la kifahari

Mwanadamu daima hufanya mipango ya muda mrefu lakini hazingatii kuwa kamba yake ya maisha iko mikononi mwa nani. Kamba ikivutwa kwa ghafla na afe, mipango yote itasambaratika. Mintarafu ya hayo, kijana mmoja kutoka Madinâ-tul-Auliyâ, Multan aliuacha mji wao na familia yake na akaenda kuishi nchi ya mbali akitafuta mali. Alikuwa akituma nyumbani pesa nyingi alizokuwa akichuma. Kulingana na makubaliano na familia yake, waliamua kumjengea jumba zuri la kifahari. Kijana aliendelea kutuma pesa kila mwaka na familia yake nayo ilimjengea jumba hilo na kulitia mapambo mpaka ujenzi ukakamilika. Kijana aliporegea nyumbani, mipango ya kuhamia jumba zuri la kifahari ilikuwa inaendelea lakini wiki moja tu kabla ya kuhamia kijana akafariki. Hivyo basi badala ya kuhamia jumba zuri la

Usiku wa Kwanza Kaburini

kifahari lenye starehe, kijana alihamishwa katika kaburi lenye giza na majonzi.

### **Wanaoleweshwa na anasa za kidunia**

Yasikitisha kuwa wengi wetu tumeleweshwa na anasa za kidunia na tumesahau kutafakari kuhusu maisha ya baadaye (ahera). Baadhi yetu tumefurahia mno anasa za ulimwengu unaoangamia hadi tumesahau maangamizi yake, kifo na tumejiingiza katika anasa za ulimwengu huu. Wengine hawana kumbukumbu kabisa za uhakika wa mauti na wanajishughulisha zaidi na kutafuta anasa na starehe za ulimwengu huu hata wamesahau mateso, giza na upweke wa kaburi. Ah! Leo nguvu zetu zote hutumika kustawisha maisha yetu ya kidunia; ni nadra kujishughulisha na maisha ya baadaye (ahera).

**Hebu tafakari kwa sekunde moja:** Watu wangapi waliokuwa na mali waliupita ulimwengu huu na kusahau upweke wa kaburini. Walijihuisha na kutafuta pesa, kutamani sifa na utukufu, kijiingiza katika anasa pamoja na jamaa na marafiki na kufurahia mno sifa za urongo wanazopewa na walio chini yao. Hata hivyo wingu la kufisha likaja, upepo wa kifo ukapiga, na matumaini ya kuishi zaidi ulimwenguni yakapasuka kama povu. Kifo kikawatenganisha na nyumba zao. Kikawaburuta kutoka majumba yao ya kifahari na kuwaingiza katika makaburi yenye giza na huzuni. Ah! Mpaka jana watu wale walikuwa katika shangwe na furaha mionganoni mwa familia yao yenye furaha kuu lakini leo wanahuzuni na uwoga wa upweke wa kaburini.

## Udanganyifu wa ulimwengu

Hakika anasikitisha yule ambaye ameghurika na ulimwengu huu na akawa amesahau kifo hata baada ya kuona kuwa ulimwengu hauna salama. Kwa yakini yule anayenaswa na udanganyifu wa anasa za ulimwengu na akasahau kifo, kaburi na kufufuliwa, na hafanyi matendo ya kumfurahisha Allah ﷺ anafaa kulaumiwa. Katika kututahadharisha na udanganyifu huu Muumba wetu ﷺ amesema katika Sūrah Fātir, aya ya 5:

يَأَيُّهَا النَّاسُ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ  
فَلَا تَعْرِضُكُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَلَا يَغُرِّنَّكُمْ بِاللَّهِ الْغَرُورُ ﴿٥﴾

“Enyi watu! Hakika, ahadi ya Allah ﷺ ni hakii, basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala yule mdanganyaji mkubwa (Iblisi) asikudanganyeni juu ya Mwenyezi Mungu.”

Enyi wapenzi wa Mtume Mtukufu na ndugu zangu wapenzi waislamu! Yule ambaye anaelewa vizuri ukweli wa mauti na matukio baada ya kifo hawezi kutamani anasa za kidunia. Umeshawahi kumuona mtu akitengeneza samani ili iwekwe kaburini? Umeshona kiyoyozi kikiwekwa kaburini? Sefu ikiwekwa ili itiwe pesa? Au makabati yakiwekwa ili kuwekea vikombe na stakabadhi za kuthibitisha ushindi wa kilimwengu wa michezo au masomo? Bado hujayaona haya na wala haikubaliwi na sheria kufanya hivi. Ikiwa tutaacha vitu hivi vyote hapa, shahada hizi zitakuwa na manufaa gani kwetu?

Usiku wa Kwanza Kaburini

Mali tulioichuma kwa tabu katika maisha yetu yote itatusaidia vipi? Mwisho, utabaka uliotufanya tuwe na dhara u na kiburi utatusaidia vipi? Ndugu waislamu wapenzi! Bado tuna muda wakutanabahi na kujityarisha kwa ahera na kaburi.

### Ishi kama msafiri katika ulimwengu huu

Imesimuliwa na Sayyidunā ‘Abdullah Ibn-e-‘Umar رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُمَا kwamba Mtume Mtukufu حَلَّ اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alinishika bega na akasema, “Ishi katika ulimwengu huu kama msafiri.” Sayyidunā Ibn ‘Umar رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُمَا alikuwa akisema, “Jioni inapoingia, usingojee asubuhi inayofuata, na asubuhi ikija, usingojee jioni. Jitayarische kwa ugonjwa wakati uko na afya na ujitatayarische na kifo wakati uko hai.” (*Sahīh Bukhārī, Juzuu ya 4 uk. 223, Hadis 6416*)

### Lengo la maisha ya ulimwenguni hasa ni kujitayarisha kwa maisha ya ahera

Katika hotuba ya mwisho ya Sayyidunā ‘Uśmān Ghānī رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ, alisema, “Allah عَزَّوَجَلَّ ametupa ulimwengu huu kwa lengo la kujitayarishia ahera yetu tu wala hakutupa ili uje utupoteze. Bila shaka ulimwengu huu utaangamia na ahera ni ya milele. Ulimwengu usije ukakusahafulisha na ahera. Usiipe kipaombele dunia yenye kuangamia dhidi ya maisha ya kudumu ya ahera kwa sababu ulimwengu utakatika na bila shaka tutaregea kwa Allah عَزَّوَجَلَّ. Mche Allah عَزَّوَجَلَّ kwa sababu kumcha Allah عَزَّوَجَلَّ ni ngao (ya kujikinga) adhabu yake na ni njia ya kumkaribia.”

(*Žamm-ud-Duniyā, Juzuu ya 5 uk. 83, Hadis 146*)

Enyi wapenzi wa Mtume na ndugu waislamu! Dunia hii ni mfano wa njia ambayo hupitiwa tu ili ufile (mwisho) ulikokusudia. Basi aidha mwisho ni peponi au motoni! Hii itategemea namna tulivyosafiri kwa mujibu wa maamrisha ya Allah ﷺ na Mtume ﷺ au kinyume chake. Kwa hivyo ikiwa tunataka kujishindia neema za peponi na kujiepusha na adhabu ya motoni basi lazima tufanye bidii kujirekebisha pamoja na watu wote wa ulimwengu.

### Tangazo la maiti

Mtume Mtukufu ﷺ amesema, “Naapa kwa Yule ambaye maisha yangu yako chini ya mamlaka yake, ikiwa watu watayaona maskani ya maiti na wayasikie maneno Yake watamsahau na watalilia maisha yao wenyewe. Maiti anapowekwa katika jeneza na kuinuliwa, roho yake hukaa juu ya jeneza kwa kukata tamaa na kuita kwa kelele, “Enyi jamaa na marafiki! Musighuriwe na ulimwengu kama ulivyonighuri mimi. Nilikusanya mali ya halali na haramu na nimewaachia wengine. Faida ni kwao wao na hasara ni kwangu mimi. Kwa hivyo pateni funzo kutokana na yale yaliyonipata mimi. (*At-tazkirâh lil Qurṭabî, uk. 76*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

### Usemi wa maiti

Inaelezwa na Sayyidunā Abū Sa'īd Khudrī رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ kwamba Mtume kipenzi aliyebarikiwa ﷺ mesema, “Wakati

watu wako tayari kwenda kuzika na maiti ameenuliwa hadi mabegani basi ikiwa maiti ni muongofu husema, “Nipelekeni haraka.” Ikiwa maiti ni muovu husema, “Ah! Munanipeleka wapi?” Viumbe wote husikia sauti yake isipokuwa binadamu na iwapo binadamu angesikia basi angeanguka na kuzimia.” (*Sahīh Bukhārī*, Juzuu 1, Uk.465, Hadis 1380)

## Wito wa kaburi

Inaelezwa na Sayyidunā Abul Ḥujjāj Šumālī رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَنْهُ ya kwamba Mtume Mtukufu حَلْقَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Maiti anapozikwa, kaburi humwambia: “Ewe mtu! Ole wako! Kwa nini ukonisahau? Je, hukujua kuwa mimi ni nyumba ya majonzi na giza? Ni kitu gani kilikufanya ukatembea juu yangu kwa kiburi?” Kama maiti alikuwa muongofu sauti italiambia kaburi, “Ewe kaburi! Je akiwa ni mionganoni mwa wale waliokuwa wakiwalingania watu katika wema na kuwakataza (kutenda) maovu, halafu? (utamfanya nini?)” Halafu kaburi litasema, “Ikiwa ni hivyo, basi nimekuwa bustani ya peponi kwa ajili yake yeche.” Halafu mwili wa mtu huyu unabadilika na kuwa Nur (mwangaza) na roho yake hupanda kwa Allah عَزَّوجَلَّ.” (*Musnad Abī Ya'lā*, Juzuu ya 6, Uk. 67, Hadis 6835)

Enyi wapenzi wa Mtume na ndugu waislamu wapenzi! Tafakarini kwa makini juu ya wakati ambapo mutaachwa peke yenu kaburini, wasiwasi utakuwa umetuaja, wala hatutaweza kwenda popote au kumuita yejote na hakutakuwa na nafasi ya kutoroka.

Wakati huo tutakaposikia sauti ya kaburi ya kupasua moyo tutafanyaje?

### **Ima ni bustani ya peponi au shimo la motoni**

Amani ya nyoyo zetu, Karimu na Mpole, Mtume wa Umma ﷺ amesema, “Aidha kaburi ni bustani kati ya mabustani ya peponi au ni shimo kati ya mashimo ya motoni.”  
(*Sunan-ut-Tirmizi*, uk. 208 Juzuu ya 4, Hadis 2468)

### **Huruma ya kaburi kwa mtiifu**

Ndugu wapenzi waislamu! Kaburini kutakuwa na faraja kwa wale waliokuwa wakisimamisha swala na wakifuata sunna ilihali kutakuwa na mateso mengi kwa wale waliokuwa wakiiga maisha ya dhambi. Kutokana na hayo ‘Allāmāḥ Imām Jalāluddīn Suyūṭī Ḥasan ibn ‘Ubayd amesema, “Imeelezwa na Sayyidunā ‘Ubaīd bin ‘Umaīr kwamba kaburi humwambia maiti, “Kama ulikuwa mnyenyeketu kwa Allah عَزَّوجَلَّ katika uhai wako basi leo nitakuhurumia na ikiwa hukuwa mnyenyeketu kwa Allah عَزَّوجَلَّ katika uhai wako basi mimi ni mateso makali kwako. Mimi ni nyumba ambayo, yule ambaye huingia akiwa muongofu na mtiifu atatoka na furaha na yule ambaye hakuwa mtiifu na mtenda dhambi, atatoka amevurugika.” (*Sharh-uṣ-Ṣudūr*, uk. 114; *Aḥwāl-ul-Qubūr li-Ibn-e-Rajab*, uk. 27)

### **Mwito kutoka makaburi jirani**

Inasemwa, “Maiti anapozikwa na kuteswa, maiti katika makaburi jirani humwita na kumwambia, “Hukupata funzo kutokana na

kifo chetu? Je, hukuona namna matendo yetu yalivyo malizika? Na ulikuwa na nafasi ya kufanya amali njema lakini uliipoteza.” Kila sehemu ya kaburi humuita na kumwambia, “Ewe uliyetembea kwa kiburi ulimwenguni! Kwa nini hukupata funzo kutokana na wale waliokufa? Je, hukuona namna gani watu walivyowainua jamaa zako waliokufa mmoja baada ya mwengine wakiwapeleka kaburini?” (*Sharah-us Sudūr*, uk. 116)

### Mazungumzo na maiti

Imetajwa katika ‘Sharḥ-us-Šudūr’, ‘Sayyidunā Sa’īd bin Maṣaib Ḥasan ibn Ḥanbal عَنْهُ amesema, “Mara moja tulikwenda maziara ya Madinah Munawwarah na Amīr-ul-Muminīn, Sayyidunā Ali-ul-Murtadā كَرِمَ اللَّهُ تَعَالَى وَجْهُهُ الْكَرِيمُ. Sayyidunā Maulā ‘Ali عَنْهُ الْمَوْلَى الْأَعْظَمُ aliwaamkua maiti kwa kuwapa salamu na akasema, “Enyi wafu (watu wa makaburini!) Mutatupa habari (za kaburi) au tuwape sisi habari? Sayyidunā Said bin Musayyab عَنْهُ الْمَوْلَى الْأَعْظَمُ alisema, “Tukasikia maneno وَعَلَيْكَ السَّلَامُ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ kutoka kaburini na mtu fulani alikuwa akisema, “Ewe Amīr-ul-Muminīn! Tupe sisi habari kuhusu kilichotendeka baada ya kifo chetu.” Sayyidunā Maulā ‘Ali كَرِمَ اللَّهُ تَعَالَى وَجْهُهُ الْكَرِيمُ halafu akasema, “Sikizeni! Mali zenu zimegawanywa, wake zenu wameolewa tena, watoto wenu wamekuwa mayatima na maadui zenu wanaishi katika nyumba mulizojinga kwa umadhubuti. Sasa twambieni kilichowafanyakia nyinyi.” Jibu likatokea kaburini, “Ewe Amīr-ul-Muminīn! Sanda zetu zimerarukararuka, nywele zetu zimenyofoka, ngozi yetu imechanikachanika, macho yetu yameanguka mashavuni

na usaha unatiririka kutoka puanī. Tumevuna kile tulichochuma na tumeputa hasara kwa kile tulichokiacha nyuma (duniani)”  
(*Sharḥ-us-Ṣudūr*, uk. 209; *Ibn-e-‘Asakir*, Juzuu ya 27, uk. 395)

### Ziko wapi nyuso hizo nzuri sasa?

Sayyidunā Abū Bakr as-Ṣiddīq ﷺ alikuwa akisema wakati akihotubu, “Wako wapi wenye nyuso nzuri? Wako wapi waliokuwa wakiringia ujana wao? Wameenda wapi wale wafalme waliokuwa wakijenga miji mizuri na mikubwa na kuimarisha kwa ngome kubwa? Wako wapi wale waliokuwa washindi vitani? Bila shaka wakati umewachakaza na sasa wamelala ndani ya giza la kaburi. Fanya hima kutenda amali njema na uombe msamaha!” (*Shu’ab-ul-Īmān*, Juzuu ya 7, uk. 365, Hadis 10595)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

### Fanya maandalizi sasa

Ndugu wapenzi waislamu! Sayyidunā Abū Bakr as-Ṣiddīq ﷺ anatuzindua kutoka kwa usingizi mzito wa kutojali kwa kututanabahisha juu ya udhaifu wa dunia hii, udanganyifu wake na giza la kaburini. Anatupa namna ya kujitayarisha kwenda kaburini na siku ya kiyama. Ni kweli mtu mwerevu ni yule ambaye hujitayarisha kwa kifo kabla ya kufa kwa kukusanya hazina ya amali njema na hupanga kuwa na mwangaza kaburini kwa kuchukua kandili ya Madani ya sunna. Tahadhari! Kaburi halimjali aliyemo ndani yake-awe tajiri au maskini, waziri au diwani wake, mtawala au mtawaliwa, afisaa au katibu, muajiri

au muajiriwa, daktari au mgonjwa, mmiliki wa ardhi au kibarua, yejote awaye; kama alikuwa na upungufu katika kujitayarisha kwa maisha ya ahera, kama alikosa sala kimakusudi, hakufunga mwezi wa Ramadhan bila sababu ya kisheria, hakutoa zaka hata ingawa ni wajibu kwake, hakuenda kuhiji Makka ingawa ililmazimu, hakujisitiri kulingana na sheria ingawa alikuwa na mamlaka ya kufanya hivyo, hakuwa mtiifu kwa wazazi wake, alikuwa na tabia ya udanganyifu, kusengenya na kutoa siri za watu, kutazama filamu na drama, kusikiliza nyimbo, kukata ndevu au kuzipunguza chini ya urefu wa ngumi; kwa kifupi, iwapo amefanya dhambi nyingi mno, basi ikitukia kwamba Allah ﷺ na Mtume wake ﷺ hawakuridhika naye atapata majuto makubwa na huzuni.

Yule ambaye ameswali swala za faradhi na akaongeza za sunna juu yake, amefunga sunna juu ya kufunga Ramadhan, alizunguka kila barabara mjini akilingania watu katika njia ya haki; Hakujifunza tu elimu ya Qurān bali aliwapa watu wengine darsa, aliweka madarasa nyumbani kwake, alisafiri pamoja na Madanī Qafilah angaa siku tatu kwa mwezi ili ajifunze sunna, alijaza kijitabu cha Madanī In'āmāt kila siku na kuwakabidhi ndugu waislamu waliowajibika katika siku 10 za mwanzo za kila mwezi wa kiislamu. Ikiwa kwa upendo na fadhila za Allah ﷺ na Mtume wake ﷺ ameondoka ulimwengu huu ilhali imani yake i salama, إن شاء الله ﷺ baraka zitamiminika kaburini mwake na chemichemi za Nur ya Mtume ﷺ zitaendelea kumulika kaburi lake.

## **Muimbaji alijiunga vipi na Dawat-e-Islami?**

Enyi wapenzi wa Mtume! Shikamaneni na mazingira ya Dawat-e-Islami wakati wote, ان شاء الله عزوجل mutafaulu duniani na ahera. Ili kukushawishi, nitakusimulia kisa cha kujenga imani. Kutokana na hayo ndugu muislamu (mwenye umri wa takriban miaka 27) kutoka Malir (Bāb-ul-Madinaḥ, Karachi) alisema, “Nilikuwa nikipenda kusoma qasida katika utoto wangu na wakati mwengine nilikuwa nikiimba katika hafla za nyumbani. Kwa kuwa sauti yangu ilikuwa nzuri, nilipata sifa nyingi kwayo ambayo ilizidisha ubinafsi wangu. Nilipokuwa mkubwa kidogo, nilikuwa na tamaa ya kujifunza kupiga gitaa na nikajiunga na chuo maalum cha mafunzo ya kuimba. Baada ya kujifundisha, kwa miaka mingi nilihusika katika mashindano mengi ya kuimba. Pia niliimba katika idhaa kadhaa za televisheni. Halafu nikabahatika kuimba katika hafla kubwa Dubai. Kutoka hapo nikasafiri hadi India kwa mashindano ya kuimba kwa takriban miezi sita. Niliimba katika hafla kubwa kubwa na filamu. Nikapata jina pamoja na utajiri mwingi. Halafu nikatembea nchi mbalimbali pamoja na kundi la waimbaji. Nilitembea Canada (Toronto na Vancouver) majimbo kumi ya Marekani (Chicago, Los Angeles, San Francisco nk.) na Uingereza (London). Niliporegea nyumbani kwa muda mfupi, jamaa zangu na majirani waliniwigia makofi. Ingawa Nafsi yangu iliayfurahia mno hayo lakini ndani ya moyo wangu sikuwa na amani na nikahisi kuna kitu fulani ambacho kimekosekana. Moyo wangu ulikuwa unatafuta utulivu wa kiroho. Nilianza kwenda msikitini

Usiku wa Kwanza Kaburini

kusali na nilibahatika kuhudhuria Darsa za Faizan-e-Sunnat zilizokuwa zikifanyika hapo baada ya Salat-ul-Isha. Darsa zilinivutia, basi nikaanza kusikiliza mara kwa mara. Hata hivyo ndoto za kwenda ng'ambo kuimba ili nipate mali na sifa zilitawala moyo na fikira zangu. Ndugu waislamu walipokuwa wakifanya ulinganizi juu yangu, nilitoa udhuru na kuondoka.

Usiku mmoja nilikwenda kulala na nikamuona mlinganizi wa Dawat-e-Islami amesimama katika sehemu iliyojuu huku akiiniita. Ilikuwa ni kama ambaye ananihimiza nitoke katika kinamasi cha dhambi nilichokuwa nimezamishwa. Nilipoamka asubuhi, nilitafakari kuhusu jinsi ninavyoishi, lakini nilibakia katika hali hiyo ya dhambi. Baada ya muda niliota tena ndoto ambayo ilinishtua kabisa! Niliona kuwa nimekufa na nilikuwa nikioshwa (josho). Halafau nikajipata Barzakh (mahali roho zinapowekwa baada ya kifo zikingojea siku ya kufufuliwa). Wakati huo nilipata hisia za kukata tamaa ambazo sijawahi kuzisikia awali. Nikajambia, “Wataka kuwa maarufu?! Sasa tazama hali yako!” Asubuhi nilipofungua macho nilikuwa nikotoka na jasho jingi na mwili wangu mzima ulikuwa ukitetemeka. Ilikuwa ni kama ambaye nimepewa nafasi ya pili kuregea duniani.

Sasa mwito wa kuimba na kutaka umaarufu nimeufutilia mbali kutoka kwa fikra zangu. Nilitubia kwa dhati na kuapa kuwa sitaimba tena. Familia yangu ilipojua waliupinga kabisa uamuzi wangu, lakini kutokana na upendo wa Allah ﷺ na Mtume wake ﷺ nilikuwa nimeshaimarisha msimamo wa Madani, kwa hivyo nikawa imara na uamuzi wangu. Nikabarikiwa

tena kumuona mlinganizi yule yule wa Dawat-e-Islami katika ndoto yangu ambaye nilimuona hapo awali. Alinihimiza. Nilipata nguvu ya Dawat-e-Islami kwa mujibu wa Aya ifuatayo ya Qur'an Tukufu:

وَالَّذِينَ جَاهَدُوا فِينَا  
لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبْلَنَا ۖ وَإِنَّ اللَّهَ لَعَلَى النُّحَسِنِينَ ﴿١٥﴾

“Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu, kwa yakini Tunawaongoza kwenye njia Zetu. Na bila shaka Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wafanyao mema.”

Nikaanza kuswali kila siku na nikapamba uso wangu kwa sunna ya ndevu iliyobarikiwa, nikapamba kichwa changu kwa kilemba cha kijani (kilemba cha Sunnah). Awali nilikuwa nikiimba mashairi ya nyimbo zenyе hisia lakini sasa imekuwa kawaida kusoma vitabu na vijitabu vilivyochapishwa na Maktaba-tul Madīnah.

Usiku mmoja nilipolala nikisoma kitabu, bahati yangu ikasimama na nikabarikiwa kumuona Mtume kipenzi ﷺ katika ndoto yangu. Shukrani zangu zote kwa Allah عَزَّوجَلَ hazifidii neema hii. Moyo wangu ulipata nguvu kutohana na hayo. Halafu kaburi lililobarikiwa la Mufti-e- Dawat-e-Islami, al-'Allāmah, al-Hafiz, al-Mufti Muhammed Fāruq Attārī عليه مُحَمَّدٌ الْقَيْ و lilifunuka kwa ajili ya mvua kali, nilifurahi mno nilipoona mwili wake ulikuwa salama na mzima, sanda yake bado hajjaharibiwa na nilipoona kilemba chake cha kijani na nywele zake nzima (hajjaharibiwa).

Nilifurahishwa mno na uzuri na fadhila za Allah na Mtume wake حَلَّ اللَّهُ عَلَيْهِ عَلِيَّوْهُ الْمَوْسَلَمْ juu ya wale ambao wameshikana na Dawat-e-Islami. Baada ya kuendelea na kazi za Madani, muimbaji wa zamani, Junaid Sheikh, leo ni mlinganizi na msomaji wa qasida wa Dawat-e-Islami kwa uzuri wa mazingira ya Madani. الحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّ وَجَلَّ, wakati wa maandiko haya, kwa bahati nilikuwa nikitoa Darsa kutoka Faizan-e-Sunnat, kuita Sadā-e-Madinaḥ (yaani kuamsha waislamu kwa sala ya alfajiri), na kushiriki katika ‘Alāqāī Daura Barā-e-Naykī kī Da’wat (ziara ya mkoa ya kulingania watu) kama Nigrān wa Zeli Mushāwarat wa Dawat-e-Islami. Allah عَزَّ وَجَلَّ anijaalie niwe imara kushikamana na mazingira ya Madani mpaka pumzi yangu ya mwisho.

آمِينٌ بِحَجَّ الْأَمِينِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَلَهُ وَسَلَّمَ

### Niliota kuhusu majina mazuri 99 Ya Allah عَزَّ وَجَلَّ

Enyi wapenzi wa Mtume na ndugu zangu waislamu! Siku chache baada ya kuandikwa kwa mambo haya ya kushangaza, muimbaji wa zamani wa kutajika Junaid Sheikh aliniambia, الحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّ وَجَلَّ “صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ عَلِيَّوْهُ الْمَوْسَلَمَ” juzi juzi nilibarikiwa tena kumuota Mtume kipenzi na akaniashiria kuhusu kujifunza majina mazuri 99 ya Allah عَزَّ وَجَلَّ. سُبْحَانَ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ Sasa nimeyahifadhi majina hayo.” الحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّ وَجَلَّ ubora wa kujifunza majina mazuri 99 ya Allah umetajwa katika Hadith lakini ni fadhila ilioye kijiwa usingizini na Mtume مَنْ يَنْهَا كُفَّارٌ فَإِنَّمَا يُنَزَّلُ مِنْ رَبِّكَ مَنْ يَتَّقِيُّ كُفَّارًا مَنْ يَنْهَا كُفَّارٌ فَإِنَّمَا يُنَزَّلُ مِنْ رَبِّكَ مَنْ يَتَّقِيُّ كُفَّارًا mwenyewe kuhimizwa naye kufanya hivyo.

Sikizeni na mufurahikie uzuri wa majina mazuri 99 ya Allah ﷺ. Mtume wa ummah, amani ya nyoyo zetu na fikira, karimu mno na mwema ﷺ amesema, “Mwenyezi Mungu ana majina 99; atakayeyahifadhi attingia peponi.” (*Şâfiîh Bukhârî*, Juzuu ya 2, uk. 229, *Hadith 2736*; Kwa maelezo zaidi tazama uk. 895-898 ya *Nuzha-tul-Qârî*, maelezo ya *Şâfiîh Bukhârî*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Ndugu waislamu wapenzi! Ninapofunga Bayan, nina bahatika kutaja ubora wa kufuata sunna na kuwawasilishia baadhi ya Sunnah na desturi. Mgawaji wa ukraimu, Mtume kipenzi ﷺ amesema, “Anayependa Sunnah ananipenda mimi, na anayenipenda mimi atakuwa nami peponi.” (*Mishkât-ul-Mâsâbîh*, Juzuu ya 1. Uk. 55, *Hadith 175*)

## Maua 14 ya Madani kuhusu Mavazi

Kwanza zingatia misemo mitatu ya Mtume kipenzi ﷺ.

1. Sitara kati ya mwili wa binadamu na macho ya jini ni kusoma unapotaka kuvua nguo بِسْمِ اللَّهِ (Al-Mu'jam-ul-Awsâf, Juzuu ya 10, uk. 173, *Hadith 10362*). Mtoaji maoni maarufu, Iħakim-ul-Ummâh, Muftî Aħmad Yār Khān عَلَيْهِ حَمْدُ الرَّحْمَنِ amesema, “Vile ambavyo ukuta au pazia inakuwa kizuizi kwa macho ya watu vile vile ndivyo ilivyo kutaja jina la Allah ﷺ itakuwa ni kizuizi kwa macho ya jini ambapo kwamba jini hataweza kumuona ye. (*Mirât-ul-Manâjîh*, juzuu ya 1. uk. 268)

2. Anayevaa nguo zake na kuomba yafuatayo, atasamehewa dhambi zake alizozifanya na atakazozifanya.

الْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِي كَسَانِي هَذَا وَرَزَقَنِي مِنْ غَيْرِ حَوْلٍ مِّنّْيَ وَلَا قُوَّةٌ<sup>١</sup>

(*Sunan Abī Dāwūd, Juzuu ya 4. Uk. 59. Hadith 4023*)

3. Anayeacha kuvalaa nguo jamala kutokana na unyenyekevu ingawa anauwezo wa kufanya hivyo, Allah ﷺ atamvisha joho la utukufu. (*Sunan Abī Dāwūd, Juzuu ya 4. Uk. 326, Hadith 4778*)
4. Kawaida mavazi matakatifu ya Mtume Mtukufu ﷺ yalikuwa ni nguo nyeupe. (*Kashf-u-li-Iltibās fīs-tihbābil-libās, uk. 36*)
5. Mavazi yatokamane na mapato ya halali. Haitakubaliwa swala ya faradhi wala ya Sunnah kama umevaa mavazi yatokanayo na mapato ya haram. (*Kashf-u-li-Iltibās fīs-Tihbābil-libās, uk. 41*)
6. Imeelezwa, “Atakayefunga kilemba chake akiwa amekaa au kuvalaa nguo zake za chini akiwa amesimama, Allah ﷺ atampiga kwa maradhi yasiyokuwa na tiba.”
7. Ukiavaa nguo, anza kutoka mkono wa kulia. Kwa mfano ukiavaa shati tia mkono wako wa kulia katika mkono wa kulia wa shati halafu mkono wako wa kushoto kwa mkono wa kushoto wa shati.

---

<sup>1</sup> Tafsiri ya dua hii: Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye amenivisha mimi nguo hizi na kuniruzuku mimi bila uwezo au nguvu zangu mwenywewe.

8. Hivyo hivyo ukivaa vazi la chini kwanza tia mguu wako wakulia kwa mguu wa kulia wa vazi halafu mguu wa kushoto kwa mguu wa kushoto wa vazi. Ukvua nguo zako fanya kinyume cha hayo yaani anza na upande wa kushoto.
9. Katika ukurasa wa 52 wa sehemu ya kitabu cha Bahar-e-Shari'at, Kitabu cha kurasa 312 kilichochapishwa na Maktabatul-Madinah, kumeandikwa, "Ni Sunnah urefu wa suruale kufikia nusu ya muundi na urefu wa mkono wa shati ikizidi sana kufikia vidole na upana wake uwe shubiri moja. (*Rad-dul-Muhtār, Juzuu ya 9. Uk. 579*)
10. Ni Sunnah kwa wanaume kuweka suruale au saruni zao juu ya kifundo cha mguu. (*Mirāt-ul-Manājīh, juzuu. 6, uk. 94*)
11. Wanaume wavae nguo za kiume na wanawake wavae nguo za kike. Tofauti hii lazima izingatiwe munapowavisha nguo watoto wadogo.
12. Katika juzuuy ya 1 ukurasa wa 481 wa Bahār-e-Shari'at, kitabu cheny kurasa 1250 kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madīnah, kumeandikwa, "Sehemu ya mwili wa mwanamume kuanzia magotini hadi chini ya kitovu ni tupu yaani kuifunika ni faradhi." (*Durr-e-Mukhtār; Rad-dul-Muhtār, juzuu ya 2. Uk. Wa 93*) Siku hizi watu wengi huva vazi la chini, kwa njia ambayo baadhi ya sehemu chini ya kitovu zinabakia wazi. (Jambo hili) ni haram. Na ikiwa robo ya sehemu yake inabakia wazi katika sala, basi sala yake itakuwa haifai. (*Bahār-e-Sharī'at*)

13. Siku hizi watu wengi huzunguka huku wakiwa wamevaa suruale fupi zinazoonyesha magoti yao na mapaja. (Jambo hili) Ni haram. Kuangalia mapaja na magoti ya mtu mwingine pia ni haram. Hususan mandhari kama hayo hupatikana ufuoni mwa bahari, katika sehemu za michezo na sehemu za kuinua vyuma; kwa hivyo mtu lazima awe muangalifu ikiwa itabidi atembelee sehemu hizo.
14. Yamekatazwa mavazi yanayoaliwa kwa kiburi. Kupambanua iwapo (mavazi) yamevaliwa kwa ari ya kiburi au la kunawenza kufanyika kwa kutafakari kama hali yako ya fikira inabakia vile vile au la kabla ya kucaa mavazi hayo. Kama itakuwa ni vile vile basi kiburi hakikuungia. Ikiwa hali ile ya mwanzo haipo basi kiburi kimeingia. Kwa hivyo jizueni kucaa mavazi kama hayo kwani kiburi ni sifa mbaya. (*Bahar-e-Shari'at, Juzuu ya 16 uk. 52; Rad-dul-Muhtār, Juzuu ya 9, uk. Wa 579*)

### Pambo la ki Madani

Pambo la ki Madani ni kuweka ndevu, kudumisha mtindo wa nywele za Mtume، صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰيْهِ وَسَلَّمَ kucaa kilemba cha kijani (kisiwe kijani cha kuiva) kucaa shati jeupe mpaka lifike nusu ya muundi kulingana na Sunnah na upana wa mikono ya shati uwe shubiri moja. Mswaki uonekane katika mfuko wa shati upande wa moyo na vazi la chini liwe juu ya vifundo vya miguu. (Ikiwa kuna kashda nyeupe juu ya kichwa na ya kahawia juu yake ni bora zaidi). Ninapomuona ndugu ye yote muislamu katika pambo la ki Madani kama lilivyoelezwa hapo juu moyo wangu hujawa

na furaha na huchanuwa kama bustani-hakika huwa bustani la Madinah!

### Dua ya Attar

Ewe Allah ﷺ nipe mimi na wale ndugu wote waislamu ambao wamejipamba kwa pambo la ki Madani tupate kifo cha ki shahidi chini ya kivuli cha kuba kubwa la kijani, tuzikwe katika Jannat-ul-Baqi na tupate ujirani wa kipenzi chako ﷺ katika Jannat-ul-Firdaus.

آمِينْ بِحَمْدِ اللَّهِ الْأَمِينْ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ

Ili kujifunza Sunnah̄ nyingi, soma machapisho mawili ya Maktaba-tul-Madīnah̄, ‘Bahār-e-Shari’at (sehemu ya 16), iliyo na kurasa 312 na ‘Sunnatayn aur Ādāb’, kilicho na kurasa 120. Njia ya shani ya kupata elimu ya Sunnah̄ ni kusafiri pamoja na Madanī Qāfilah̄ za Dawat-e-Islami pamoja na wapenzi wa Mtume ﷺ.

*Sīkhnay sunnatayn Qāfilay mayn chalo  
Lūtnay rahmatayn Qāfilay mayn chalo  
Ḩongī hal mushkilayn Qāfilay mayn chalo  
Pāo gay barakatayn Qāfilay mayn chalo*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## I AM THE WORST PERSON

1. Sayyidunā ‘Ušmān al-Ghanī رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ stated that there are five signs of a pious person:
2. He remains in good company.
3. He protects his tongue and private parts.
4. He considers the pleasures of the world as a nuisance and the religious blessing as a divine mercy.
5. He does not fill his stomach even with Ḥalāl food for fear that perhaps a little Ḥarām may have been included in it.
6. Besides himself, he considers every Muslim absolved in the Hereafter while he considers only himself as a sinner and fears from torment. (*Al Munabihāt*, p. 59)

صَلُّوْزَا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## Baraka Za Sunna

Katika mazingira mazuri ya Dawat-e-Islami (Shirika la Kimataifa la Kueneza Mafundisho ya Quran na Sunna lisilojihusisha na siasa) sunna za Bwana Mtume حَلَّ اللَّهُ كَفَلَ عَلَيْهِ دَلَلٌ zinafunzwa kwa wingi.

Ni ombi kwa kila muislamu kuhudhuria na kukesha usiku mzima kwa nia ya kutaka radhi za Allah عَذَابَهُ pamoja na niya zingine nzuri katika ijtimai ya kila wiki siku ya Alhamisi baada ya sala ya Magharibi inayofanyika katika mji anaoishi. Vile vile ni ombi kwa kila muislamu kusafiri na wapenzi wa Mtume حَلَّ اللَّهُ كَفَلَ عَلَيْهِ دَلَلٌ katika Madani Qafila kwa nia ya kupata thawabu na kujifunza sunna za Bwana Mtume حَلَّ اللَّهُ كَفَلَ عَلَيْهِ دَلَلٌ. Na afanye Fikr-e-Madina (kujisaili mwenyewe) kwa kujaza kadi ya Madani In'amaat na amkabidhi Zimmedaar (msimamizi) wake katika siku kumi za mwanzo za kila mwezi. Kwa Baraka ya kufanya hivyo أَنْ شَاءَ اللَّهُ تَعَالَى tutaweza kushikamana na sunnah za Mtume حَلَّ اللَّهُ كَفَلَ عَلَيْهِ دَلَلٌ na tutachukia maasi na tutazidi kuwa na hamu ya kulinda imani yetu.

Kila muislamu aweke azma ya kwamba: "Nitajaribu kujisuluhisha mwenyewe na watu wa ulimwengu mzima" أَنْ شَاءَ اللَّهُ تَعَالَى

Kwa ajili ya kujisuluhisha mwenyewe nita fuata Madani In'amaat na kuwasuluhisha watu wa ulimwengu mzima nita safiri katika Madani Qafilah أَنْ شَاءَ اللَّهُ تَعَالَى.

